

# **Mpango wa Kansas wa Usaidizi wa Stima kwa wenye Mapato ya Chini (LIEAP)**

## **MAHITAJI MUHIMU YA KUSTAHIKI Mpango wa Usaidizi wa Stima kwa wenye Mapato ya Chini**

Januari 2008

Mpango wa Usaidizi wa Stima kwa wenye Mapato ya Chini (LIEP) ni mpango uliodhaminiwa na serikali ambao husaidia kaya zinazostahiki kulipa sehemu ya gharama ya stima ya kaya yao kwa kutoa **manufaa ya mara moja kila mwaka**.

### **Muda wa Maombi**

**Muda wa maombi wa mwaka wa 2008 ni kuanzia Januari 22 hadi Machi 31, 2008.**

### **[Fomu ya Maombi ya LIEAP Inayoweza Kuchapishwa \(PDF\)](#)**

Muhtasari ufwatao unafafanua matoleo muhimu ya kustahiki LIEAP. Habari zaidi zinaweza kupatikana kwa kuwasiliana na Ofisi yako ya mtaaani ya Huduma za Jamii na Urudishaji wakati wa muda wa maombi wa miezi mitatu.

### **Watu Wanaostahiki**

Ndiposa uweze kustahili, waombaji lazima wafikie mahitaji yafwatayo:

- 1) Mtu mzima anayeishi kwa anwani hiyo lazima mwenyewe awe na uwajibikaji wa kununua gharama ya kupasha joto iliyopatikana katika makao ya sasa, inayolipwa aidha kwa kabaila au muuza mafuta.
- 2) Waombaji lazima waonyeshe historia ya hivi karibuni ya malipo kuwadia kununua nguvu asili ya kupasha joto. Kila Malipo lazima yawe asilimia 10 au mapato taslimu ya kila mwezi ya mwombaji au \$ 40 (yoyote ambayo ni chini) kwa miezi 2 ya miezi 3 kabla ya maombi.
- 3) Mapato taslimu yaliyochanganywa (kabla ya mikato) ya watu wote wanaoishi katika anwani hiyo haiwezi kupitisha asilimia 130 ya kiwango cha serikali cha umasikini kulingana na maongozi yaliyoorodheshwa hapo chini:

**Watu wanaoshi  
katika Anwani hiyo  
Mwezi**

**Upeo wa Mapato Unaoruhusiwa kila**

1	\$1,107
2	\$1,484
3	\$1,861
4	\$2,238
5	\$2,615
6	\$2,992
7	\$3,369
8	\$3,746
9	\$4,123
10	\$4,500
11	\$4,877
12	\$5,254
+	

ongeza \$377 kwa kila mtu wa ziada

**Manufaa**

Viwango vya manufaa vinalingana kulingana na mambo yafuatayo: 1) Mapato ya kaya, 2) idadi ya watu wanaoishi katika anwani hiyo, 3) aina ya makao, 4) aina ya mafuta ya kupasha joto, na 5) kiasi cha matumizi.

Kwa habari zaidi au kuomba fomu ya maombi, tafadhali piga simu 1-800-432-0043.